

MRADI WA BOOST KUBORESHA ELIMU YA AWALI NA MSINGI

Jumla ya vyumba vya madarasa 12,000 vya shule za awali na Msingi za Serikali hapa nchini vinatarajiwa kujengwa kwa kipindi cha miaka mitano kupitia mradi wa BOOST kwenye maeneo yenye upungufu au msongamano wa wanafunzi.

Thamani ya mradi huo ni Tsh Trilioni 1.15 kwa nchi nzima, fedha hizo zikitolewa na Serikali pamoja na Bank ya Dunia.

Utekelezaji Mradi wa BOOST

Mradi wa BOOST ni mradi wa kuimarisha na kuboresha elimu ya awali na msingi hapa nchini. Mradi huu unatekelezwa hapa nchi kwa miaka 5 kuanzia sasa hadi mwaka 2025/2026 na kunufaisha Halmashauri zote 184 hapa Tanzania hususani katika kuboresha miundombinu ya elimu kwa Madarasa ya awali na Msingi.

Mradi huu wa BOOST unatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania na kusimamiwa na Ofisi ya Raisi Tamisemi pamoja na Wizara ya Elimu Sayansi na Technologia.

Aidha mradi huu unatekelezwa kwa mfumo wa lipa kulingana na matokeo yanayopatikana na Halmashauri ambazo zitatimiza vigezo kwa kiwango kikubwa ndizo zitanufaika zaidi kwa kupatiwa fedha nyingi za kuboresha miundombinu pamoja na ununuzi wa vifaa na vitendea kazi kwa Elimu ya awali na Msingi.

Malengo ya Mradi wa BOOST

- Kuboresha Miundombinu kwa Madarasa ya awali na Msingi kote nchini.
- Kuongeza uandikishaji wa Watoto wa Elimu ya awali kutoka asilimia 76.9 ya sasa hadi asilimia 85 ifikapo mwaka 2025/2026.
- Kuimarisha mapito ya Wanafunzi wa awali na Msingi kwa kuweka mpango wa Shule salama.
- Kuimarisha na kuboresha mpango wa mafunzo endelevu kazini kwa walimu wa madarasa ya awali na Msingi mashuleni.
- Kuboresha mpango wa ununuzi wa vifaa vya kisasa vya Tehama Mashuleni hususani katika vituo teule vitakavyoainishwa katika kila Halmashauri ili kuwajengea uwezo Walimu wa shule za Msingi kujua namna bora wa upatikanaji wa masomo rejea kwa gharama nafuu ya kutumia mitandao ya Kisasa.

KAZI IENDELEEE